# Global Schools Program

MALENGO YA MAENDELEO ENDELEVU




# Muhtasari wa Kozi

## Darasa la 9

---

**Chanzo:** Reimers, F. (2017). *Empowering students to improve the world in sixty lessons*. Toleo la kwanza. Createspace Independent Publishing Platform.

**Haki ya kunakili:** © 2017 Fernando M. Reimers. Kazi hii imeidhinishwa chini ya leseni ya kimataifa ya Creative Commons Attribution 4.0. Ili kuona nakala ya leseni hii, tembelea https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/ Haki zote zimehifadhiwa.

**Taarifa:** Maudhui yote yaliyomo humu yameandaliwa na kuchapishwa kwa kujitegemea na Programu ya Shule za Kimataifa (Global Schools Program).

---

SUSTAINABLE DEVELOPMENT GOALS
17 GOALS TO TRANSFORM OUR WORLD

Global Schools Program

| Muhtasari | |
|---|---|
| **Lengo kuu la ujifunzaji**<br>Darasa la 9, wanafunzi watachunguza mada zinazohusu haki za wanawake na usawa wa kijinsia kupitia fasihi. Kwa kutumia taswira za kifasihi za wanawake, wanafunzi watachunguza kutokuwepo na usawa wa kijinsia katika maeneo yao, nchini na ngazi ya kidunia. Hatimaye , wanafunzi watabuni, kutekeleza na kuwasilisha mradi unaojikita katika yale waliyojifunza. | |
| **Nguzo za Somo** | |
| **Somo 1** | Kuangalia Fasihi: Namna gani wanawake wanatizamwa katika Muktadha wa Kiulimwengu? |
| **Somo 2** | Kuchambua Fasihi: Namna gani Wanawake wanatizamwa na Jamii zao? |
| **Somo 3** | Kujifunza kutoka kwenye Fasihi: Uhalisia wa Sasa wa Wanawake kwenye Jamii |
| **Somo 4** | Kubuni Mradi wa Kushughulikia kutokuwepo kwa Usawa wa Kijinsia |
| **Somo 5** | Kutekeleza Mradi |
| **Malengo ya Ujifunzaji** | |
| • Wanafunzi watafanyia mazoezi usomaji wa kina kadiri wanavyoendelea kuchunguza masuala ya kijamii kupitia fasihi.<br>• Wanafunzi watachukua mafunzo kutoka kwenye kazi za fasihi na kuyatumia katika maisha yao wenyewe.<br>• Wanafunzi watabuni na kutekeleza mradi binafsi kutokana na yale waliyojifunza. | |

**Darasa la 9 Somo 1**

"Harakati za Haki za Wanawake: Kujiweka/Kuzama kwenye Fasihi"

**Muda:** dakika 60
**Masomo:** Maarifa ya Jamii, Uraia, Historia
**Viwango:** Usawa wa Kijinsia na Uwezeshaji wa Wanawake na Wasichana (MME 5); Uboreshaji Usawa (MME 10); Amani, Haki na Taasisi Imara (MME16)
**Limebuniwa na:** Matt Owens

**Ufupisho na Mantiki:** kutoa muundo wa kijamii na kihistoria kama msingi wa masomo yanayofuata ambapo wanafunzi watachunguza harakati za usawa wa kijinsia na haki za wanawake kupitia hadithi fupi na mashairi.

**Malengo ya uelekezaji:**

- Wanafunzi watapata utambuzi mkubwa wa harakati za haki za wanawake katika historia, kuunda muktadha kupitia fasihi zitakazosomwa kwenye masomo yajayo.
- Wanafunzi watajenga msingi utakaowaruhusu kusoma hadithi zao fupi au shairi wakiwa na jicho la udadisi.

**Malengo ya Umahiri:**

- Harakati za haki za wanawake zina historia imara ,mahiri na yenye nafasi katika jamii ya kimataifa hivi leo.
- Harakati za haki za wanawake kutoka kote ulimwenguni zimefanya kazi bila kuchoka kuongelea ukosefu wa usawa katika jamii kipindi chote cha historia na hata leo zipo.

**Maswali muhimu:**

- Wanawake wamekumbana na ukosefu wa usawa upi katika historia na sasa?
- Jinsi gani wanawake na harakati za haki za wanawake zimekabiliana na ukosefu wa usawa kipindi chote cha historia?
- Misukumo gani mikubwa ya kijamii na kihistoria imepelekea kuibuka kwa harakati za haki za wanawake?
- Ni Jinsi gani fasihi inaweza kutumiwa kama lenzi (kioo) sahihi ya kutathmini masuala ya haki za wanawake?

**Malengo ya ujifunzaji kwa mwanafunzi (wanafunzi watakuwa na uwezo wa):**

- Kushiriki kwenye mjadala muhimu unaohusu jukumu na mchango wa harakati za haki za wanawake katika kuzungumzia ukosefu wa usawa wa kijinsia.

- Kutengeneza mfumo muhimu wa kuunganisha uhusiano wa fasihi watakazosoma katika madarasa yanayofuata .

**Upimaji:** Majadiliano ya darasani

**Mtiririko wa shughuli:**

- **Utangulizi (dakika 10):** Mwalimu atatoa utangulizi mfupi wa harakati za haki za wanawake katika kipindi chote cha historia hadi sasa, pamoja na harakati ulimwenguni kote.

- **Usomaji wa vyanzo vya msingi (dakika 20):** mwalimu atawapanga wanafunzi katika makundi madogo na kuwagawia machapisho ya vyanzo vya msingi. Wanafunzi watatumia dakika 10 za kwanza kusoma kimya kimya. Halafu watajadili katika makundi madogo maswali yanayoulizwa na mwalimu. Ni ukosefu wa usawa upi au mvutano gani walioubaini wanafunzi? Kwa jinsi gani mambo hayo yanaweza kushughulikiwa?

- **Majadiliano ya darasani (dakika 20):** wanafunzi watakusanyika tena darasani ili kujadili makala tofauti tofauti, maudhui yaliyojitokeza kote na tamaduni tofauti . Mwalimu anaweza kuyapanga makundi upya ili wanafunzi waweze kujadili na wanafunzi wengine waliosoma kazi tofauti.

- **Fasihi (dakika 10):** Mwalimu kuwasilisha nakala tofauti tofauti ambazo wanafunzi watasoma kwa ajili ya uchambuzi wa fasihi. Wanafunzi kuchagua nakala watakazosoma kwa ajili ya kipindi kijacho.

**Nyenzo kwa walimu:**

- https://rfkhumanrights.org/our-programs/speak-truth-to-power/lesson-plans?topic=25708
- https://interactive.unwomen.org/multimedia/timeline/womenunite/en/index.html?gclid=CjwKCAjwtuOlBhBREiwA7agf1gmgQt6YLv7kT6hFbTx-P_mULwKtfMNPLWadd7fTNLdzQWzJ0-T8NBoCB7YQAvD_BwE#/1840
- https://interactive.unwomen.org/multimedia/timeline/womenpeacesecurity/2020/en/index.html

**Darasa la 9 Somo 2**

“Kuchambua Fasihi: Wanawake Wanapewa taswira gani kwenye Jamii zao?”

**Muda:** dakika 50
**Masomo:** Maarifa ya Jamii, Fasihi
**Viwango:** Usawa wa Kijinsia na Uwezeshaji wa Wanawake na Wasichana (MME 5)
**Limebuniwa na:** Cassie Fuenmayor

**Ufupisho na Mantiki:** somo hili litajikita kwenye uchambuzi wa fasihi ambayo wanafunzi walichagua kwenye somo la kwanza. Watachambua wakiwa (kwenye makundi) njia ambazo wanawake wanawasilishwa ndani ya fasihi, na vile vile vipengele vya fasihi vinavyounda/kuchangia uwakilishi huu.

**Malengo ya uelekezaji:**

- Wanafunzi watakuza uthamini, udadisi, na heshima kwa utofauti wa kitamaduni.
- Wanafunzi watafanya mazoezi ya ustadi wa kufikiri kwa kina na uchanganuzi huku wakitazama ushairi/riwaya/hadithi fupi.

**Malengo ya Umahiri:**

- Kukuza uthamini, udadisi, na heshima kwa utofauti wa kitamaduni na utamaduni wa ulimwengu kama msingi wa kujitafakari, kuunda utambulisho, na kukaribia muingiliano wa kibinadamu.
- Kuanzisha msingi thabiti katika historia ya ulimwengu, jiografia na utamaduni, na pia kuchunguza fasihi ya kiulimwengu.
- Kuhoji miundo ya kimadaraka iliyopo na kutambua nafasi yake ndani ya muktadha mahususi wa ulimwengu.
- Kuelewa utambulisho na chimbuko lake binafsi, utambulisho na machimbuko ya wengine, jinsi utamaduni unavyotambulisha watu, na mahali ambapo mtu yuko katika nafasi na wakati.
- Kutambua ubaguzi wa kitamaduni na namna ya kupunguza athari zake.
- Kuelewa jinsi maadili yanavyoundwa kupitia utamaduni, dini, na uzoefu.
- Kuelewa njia ambazo fasihi inaweza kuwakilisha pasipo usahihi na kwa usahihi hali halisi za kijamii na kitamaduni

**Maswali muhimu:**
- Jinsi gani wanawake wanawakilishwa katika fasihi uliyosoma?
- Je, hii inategemeanaje na muktadha/muundo wa fasihi au mwandishi?
- Je, uwasilishwaji huu wa wanawake unatuonyesha nini kuhusu tamaduni mbalimbali?
- Je, tunaona ukosefu wowote wa usawa au kutokuwepo usawa wa madaraka katika fasihi hii?

**Malengo ya ujifunzaji wa mwanafunzi (wanafunzi watakuwa na uwezo wa):**
- watamaliza somo wakiwa na uelewa wa jinsi wanawake wanavyowakilishwa katika muktadha wa fasihi waliyosoma.
- kufikiria juu ya njia ambazo fasihi ilionyesha kwa usahihi na kwa isivyo sahihi na uhalisia wa kitamaduni

**Upimaji:** Mwalimu anaweza kuzunguka na kufuatilia mijadala ya vikundi.

**Mtiririko wa shughuli:**

- **Sehemu ya 1 (dakika 25):** Wanafunzi watakaa katika makundi madogo madogo ili kujadili kazi yao ya fasihi waliyochagua:
    - Je, unajua nini kuhusu muundo/muktadha/mwandishi wa fasihi unayosoma?
    - Je, wanawake wanawakilishwa vipi katika fasihi uliyosoma?
    - Je, uwakilishwaji huu unategemeanaje na muktadha/muundo wa fasihi au mwandishi?
    - Je, uwakilishwaji huu wa wanawake unatuonyesha nini kuhusu tamaduni mbalimbali?
    - Je, tunaona ukosefu wowote wa usawa au wa madaraka katika fasihi hii?
    - Je, unafikiri uwakilishwaji huu ni sahihi kwa muktadha?

- **Sehemu ya 2 (dakika 25):** Wanafunzi watakaa katika makundi mbalimbali ili kushiriki kuhusu fasihi waliyosoma na kundi ambalo halikuisoma. Mara tu kila mtu atakaposhiriki, wanafunzi watajibu maswali ya majadiliano yafuatayo:

    - Je, unaona mfanano/tofauti zozote kati ya njia ambazo wanawake wanawakilishwa?
    - Katika muktadha upi wanawake wanawasilishwa kwa njia chanya/hasi?

**Darasa la 9 Somo 3**

"Uunganishaji wa fasihi na uhalisia: Wanawake kwenye Jamii  Yetu"

**Muda:** dakika 50-60
**Masomo:** Fasihi, Maarifa ya Jamii
**Viwango:** Usawa wa Kijinsia ,Uwezeshaji wa Wanawake na Wasichana (MME 5); Uboreshaji Usawa (MME 10); Amani, Haki na Taasisi Imara (MME 16)
**Limebuniwa na:** Heather Kesselman

**Ufupisho na Mantiki:** Wanafunzi watafanya miunganisho kati ya mada za uwezeshaji wa wanawake katika fasihi na nafasi ya wanawake katika maisha yao na jamii. Hii ni muhimu katika kubinafsisha fikra za usawa wa kijinsia katika muktadha maalum.

**Lengo la uelekezaji:** Wanafunzi wataweza  kuunganisha fasihi na hali halisi ya sasa katika jamii zao.

**Malengo ya ujifunzaji:**

- Fasihi inaweza kuiga maisha na kuakisi ukosefu wa usawa wa kijamii katika ulimwengu wetu.
- Nafasi ya mwanamke katika jamii ni tata na kimsingi haina usawa.

**Maswali muhimu:**

- Je, ni kwa jinsi gani njia ambazo wanawake wanawakilishwa katika fasihi zinaonekana au hazionekani katika jamii yako mwenyewe?
- Ni kwa njia zipi  wanawake wanatendewa isivyo haki katika jamii yako?
- Je, ni miundo gani ya msingi ya kimadaraka na maadili ya kitamaduni ambayo yanafafanua jinsi wanawake wanavyotendewa/wanavyowakilishwa katika jamii yako?

**Malengo ya ujifunzaji wa mwanafunzi  (wanafunzi watakuwa na uwezo wa):**

- Kuchambua ukosefu wa usawa wa kijinsia katika jamii zao.
- Eleza mfanano na tofauti kati ya nafasi mbalimbali za wanawake katika fasihi.

**Upimaji:** Bango dogo na tafakuri ya mwisho
**Mtiririko wa shughuli:**

- **Uandishi huru (dakika 5):** wanafunzi wanaeleza kwa maandishi juu ya mwanamke muhimu maishani mwao au katika jamii zao. Ana madaraka gani? Ana mahangaiko gani?

- anayokumbana nayo? Ni matarajio gani ya kijamii au kitamaduni yanayomzuia au kumpa madaraka? Ni machaguo gani anayoweza kufanya na ni machaguo yapi yatafanywa kwa ajili yake? Je, maisha yake au fursa zingekuwa tofauti kama angekuwa mwanaume?

- **Mazungumzo katika jozi (dakika 5):** wanafunzi wanaeleza hadithi ya mwanamke waliomchambua na wenzao, wakijadili swali "Jinsi gani jinsia yake inachochea fursa zake, machaguo, mwenendo, na malengo yake?"

- **Mazungumzo ya kundi zima (dakika 5):** wanafunzi 2-3 wanashirikishana walichojadili na wenzao.

- **Uchambuzi wa matini (dakika 20):** , wanafunzi wawili wawili wakusanye mifano ya angalau nukuu 5 au visa kutoka kwenye fasihi inayozungumzia nafasi ya wanawake kwenye hadithi, na waandike haya na makisio/uchambuzi pembeni ya kila mfano. Hii inaweza kufanywa katika mfumo wa Cornell Notes, michoro ya visanduku vya maandishi itakayochaguliwa na mwalimu au jedwali la mpangilio katika madaftari ya wanafunzi.

- **Shiriki Matokeo (dakika 3):** wanafunzi wanataja baadhi ya mifano waliyopata, wanalinganisha taarifa zinazofanana na zinazofautiana. Hii itawasadia wanafunzi wanaopata ugumu kujaza nafasi zilizo wazi kwenye chambuzi zao.

- **Uundaji wa zana maono (dakika 10):** wanafunzi wanaunda kielelezo cha Venn au kielelezo maandishi chochote walichochagua kulinganisha nafasi ya wanawake katika fasihi na ile ya kwenye jamii zao wenyewe.

- **Uwasilishaji na Maonesho ya kazi za sanaa (dakika 3):** Wanafunzi wanazungukia makundi ya wenzao kutazama maudhui yanayojitokeza mara kwa mara, yanayotambuliwa na wanafunzi wenzao.

- **Tafakuri ya mwisho (dakika 8):** wanafunzi watajibu katika madaftari yao maswali yafuatayo: "Mfanano au tofauti gani tunaweza kuziona kati ya nafasi ya wanawake kwenye fasihi na katika jamii zetu?"

**Nyenzo (zana) kwa mwalimu:**

- karatasi ya kazi ya kielelezo cha Venn: https://www.canva.com/graphs/venn-diagrams/
- https://www.canva.com/graphs/templates/venn-diagram/

**Darasa la 9 Somo 4**

"Kubuni Mradi wa Kuongelea kutokuwepo kwa Usawa wa Kijinsia"

**Muda:** dakika 50-120
**Masomo:** Fasihi, Maarifa ya Jamii
**Viwango:** Usawa wa Kijinsia na Uwezeshaji wa Wanawake na Wasichana (MME 10); Amani, Haki na Taasisi Imara (MME 16)
**Limebuniwa na:** Christian Bautista

**Ufupisho na mantiki:** Katika kipindi hiki, wanafunzi watabuni kazi ya sanaa inayozungumzia ukosefu wa usawa wa kijinsia katika jamii za wanafunzi zenyewe. Kazi hii inaweza kuwa hadithi fupi, shairi, picha za kuchorwa kwa rangi, michoro, uchongaji, wimbo, utunzi, n.k. Somo hili linaweza kupangwa kwa kushirikiana na mwalimu wa sanaa za ubunifu au maonesho.

**Lengo la uelekezaji:** wanafunzi watatumia ubunifu wao katika suala la kijamii kwenye maisha yao wenyewe au jamii zao katika njia ya kushabihisha kazi zao kwenye masomo yaliyopita na kuwashirikisha wadau nje ya darasa.

**Malengo ya uelewaji:**

- Sanaa za ubunifu na maonesho kama njia ya kuanzisha harakati za kijamii.
- Masuala halisi ya kijamii na kisiasa yanaweza kuzungumzwa na vijana na wanafunzi wanapochukulia ubunifu na maonesho  kwa uaminifu, umoja na ubunifu.

**Maswali muhimu:**

- Namna gani sanaa inaweza kuwakilisha ukosefu wa usawa tuliochunguza katika masomo yaliyopita?
- Je, mbinu za kisanii ni za kipekee sana katika kufuatilia haki za jamii?
- Ni nini nguvu/mapungufu ya/za kila aina ya zana (picha za kuchorwa kwa rangi, uimbaji, n.k.) katika kufuatilia/kufanikisha upatikanaji wa haki za jamii?
- Jinsi gani sanaa inaweza kuumba utamaduni na jamii?

**Malengo ya ujifunzaji wa mwanafunzi (wanafunzi watakuwa na uwezo wa):**

- Kuunda kazi halisi za sanaa zinazoakisi masomo binafsi waliyojifunza katika Somo 1-3.
- Kuelezea kupitia maandishi au tafakuri ya mdomo kwanini wamefanya maamuzi ya kisanii waliyoyafanya.

**Upimaji:** Uwasilishaji wa kazi ya sanaa iliyoandaliwa ; tafakuri ya maandishi au ya mdomo.

**Mtiririko wa shughuli:**

- **Uhusiano kati ya Matini na Uandishi huru (dakika 5-7):** wanafunzi wanaandika kwa uhuru kuhusu maendeleo yoyote wanayofikiria katika vipindi 2 vya kwanza. Inawapasa warudie nukuu 5 ambazo walikusanya kutoka Somo la 3 na vile vile nukuu zozote kutoka kwa wanafunzi wenzao ambazo zimewavutia, na pia watafakari juu ya uhalisia wa nukuu hizi katika maisha yao wenyewe na jamii zao .

- **Uandaaji wa kazi za a sanaa (dakika 20-60):** ni lazima wanafunzi watumie muda uliotengwa kutengeneza kazi zao za sanaa ambazo zinajaribu kupambana na moja au zaidi ya maswali haya muhimu:
    - Ni ukosefu wa usawa upi ambao wanawake hasa katika jamii yetu wamekumbana nao katika historia na hivi sasa?
    - Jinsi gani jamii imejibu kuhusu ukosefu wa usawa katika kipindi chote cha historia?
    - Je, kuna njia ya kisanii ya kuchora misukumo mikubwa ya kijamii na kihistoria ambayo imeumba(imesababisha) kuibuka kwa harakati za haki za wanawake?
        - Kama wanafunzi wanatengeneza michoro ya kutumia rangi, picha za vyumba vyumba, au kazi nyinginezo za sanaa ya kuona, inapendekezwa kuwa mwalimu aweke mipaka kwa njia ya kisanii watakayokubaliana, kulingana na upatikanaji au fursa ya kushirikiana na mwelekezaji mwingine (mwelekezaji/mwezeshaji wa muziki, mwelekezaji/mwezeshaji wa sanaa n.k.)
            - Zana zinazopendekezwa:
                - Mkusanyiko wa picha za mwanafunzi mwenyewe au picha za gazeti la eneo hilo, kutoka kwenye tovuti, n.k.
                - Aina yoyote ya picha za kuchorwa kwa rangi, labda zenye mipaka fulani (kutumia rangi 2 pekee n.k.)
                - Picha, ushairi, uandishi wa kusimulia, uandishi wa nyimbo

- **Tafakuri ya mwisho (dakika 20):** Kulingana na asili ya zana, aidha wanafunzi watumie muda kuandika majibu ya moja kati ya maswali muhimu hapo juu au wawasilishe kwa njia ya mdomo kazi zao mbele ya darasa zima. Kama miradi ni mikubwa (au imetumia zaidi ya kipindi kimoja kutengeneza) mwalimu afikirie kuwa na tukio kando ili wanajamii (walimu, watawala, na wazazi) waalikwe kuona kazi za wanafunzi.

**Darasa la 9 Somo 5**

"Utekelezaji wa Mradi"

**Muda:** dakika 120-180
**Masomo:** Fasihi, Sanaa, Maarifa ya Jamii
**Viwango:** MME 5 (Usawa wa Kijinsia na Uwezeshaji wa Wanawake na Wasichana); MME 10 (Uboreshaji wa Usawa); MME 16 (Amani, Haki na Taasisi Imara)
**Limebuniwa na:** Chihiro Yoshida

**Ufupisho na Mantiki:** kutumia kazi za sanaa ambazo wamezitengeneza katika Somo la 4 kama zana, wanafunzi wataonesha kwa jamii pana zaidi katika eneo la umma na kuongoza majadiliano juu ya mada ya ukosefu wa usawa wa kijinsia ambao unaweza kuwepo katika jamii.

**Lengo la uelekezaji:** wanafunzi watawasilisha na kusambaza kazi zao kwa jamii pana zaidi, kufanya mazoezi ya kuzungumza mbele ya hadhara, na kujifunza kuwashirikisha wanajamii wengine katika majadiliano kuhusu masuala ya kijamii.

**Malengo ya uelewaji:**

- Sanaa za maonesho na ubunifu kama zana inayojieleza inaweza kutumika kama mahala pa kuanzia kwa harakati za kijamii.
- Masuala halisi ya kijamii na kisiasa yanaweza kuzungumzwa na vijana na wanafunzi wanapotenda kazi za sanaa  kwa uaminifu, umoja na ubunifu.
- Kujihusisha katika mazungumzo na wanajamii inaweza kuwa na chachu  ya msukumo wa kichukua hatua.

**Maswali muhimu:**

- Jinsi gani Vijana wanaweza kuzipa changamoto fikra za ukosefu wa usawa wa kijamii na kijinsia?
- Jinsi gani sanaa inaweza kutumika kama njia ya kuhamasisha na kushirikisha jamii kwa upana ili kushiriki katika mijadala ya masuala ya kijamii?
- Nani ni wadau ndani ya jamii inayowazunguka ambao ni lazima washirikishwe katika mazungumzo kwa ajili ya kuanzisha hatua zaidi?

**Malengo ya ujifunzaji kwa mwanafunzi (wanafunzi watakuwa na uwezo wa):**

- Kufanya mazoezi na kujifunza kuzungumza mbele ya hadhara kubwa.
- Kujifunza kuongoza mazungumzo na wadau wa masuala ya kijinsia.

**Mtiririko wa shughuli:**

- **Chemsha bongo (dakika 60):** wanafunzi kufanya kazi katika jozi au makundi madogo ili kutafakari kazi za sanaa walizotengeneza na kujadili njia ya ufanisi ya kuwasilisha na kuonyesha kwa wanajamii. Wanaweza kuchagua:
    - Kuongezea maelezo ya kimaandishi ili kuelezea kazi zao za sanaa;
    - Kufanya onesho fupi la kazi hiyo;
    - Kuelezea kazi zao za sanaa kwa wageni ambao wanatembelea mabanda.

- **Uwasilishaji (dakika 20):** kazi ya sanaa itashirikishwa katika tukio la kadamnasi, lililoandaliwa katika maktaba ya umma, shirika la kijamii, bustani, n.k. ambalo linaweza kuwavutia wanajamii wengi kutembelea na kushiriki pamoja na wanafunzi. Shule na walimu watafanya kazi na taasisi na wenyeji kuandaa tukio, wanafunzi watawasilisha kazi zao za sanaa kwa wageni.

- **Mjadala (dakika 40):** wanafunzi na wanajamii kukaa katika makundi madogo ya majadiliano ili kushiriki katika mazungumzo (yanayoongozwa na wanafunzi) kuhusu kazi ya sanaa na ukosefu wa usawa wa kijinsia wanaotaka kuzungumzia. Baadhi ya maswali ya mwongozo ni:
    - Hiyo Kazi ya sanaa iliibua hisia gani ndani yako?
    - Je, unakubaliana/hukubaliani na jumbe za hiyo kazi ya sanaa?
    - Jinsi gani baadhi ya sauti zinaweza kuachwa nje katika mjadala?
    - Namna gani jamii inaweza kuboresha uzungumziwaji wa masuala haya ya jinsia?
    - Unadhani nafasi yako inaweza kuwa ipi kwenye jitihada hii?

- **Tafakuri (dakika 15):** Wanafunzi watarudi darasani ili kushiriki katika mjadala na kutoa walichojadili na wanajamii, na namna wanavyoweza kuendeleza ari. Wanaweza pia kushiriki katika tafakuri binafsi kupitia kuandika katika shajara.

**Nyenzo kwa walimu:**

- Mwongozo wa Kuwawezesha Vijana kuwa Watetezi wa Usawa wa Kijinsia: https://developmenteducation.ie/resource/through-the-looking-glass-a-guide-to-empower-young-people-to-become-advocates-for-gender-equality/
- https://www.unwomen.org/en/news-stories/press-release/2023/03/women-in-power-in-2023-new-data-shows-progress-but-wide-regional-gaps